


Kutafakari Kuhusu Sheria za Nyumbani

Tumia daftari hili kutafakari kuhusu sheria zilizo ngumu kwako kutii. Pia, unaweza kulitumia kama msingi wa mazungumzo pamoja na wazazi wako.



▶ Kwa nini huipendi sheria hiyo?


▶ Kuna sehemu yoyote ya sheria hiyo unayoweza kukubaliana nayo?

▶ Unafikiri ni kwa nini wazazi wako waliweka sheria hiyo?

▶ Je, unafikiri wazazi wako hawakuzi-ngatia jambo fulani walipoweka sheria hiyo? Ikiwa ndivyo, ni jambo gani?

► Ungependa warekebishe jambo gani katika sheria hiyo?

Unafikiri ikiwa ungewaomba wazazi wako warekebishe sheria hiyo, wangeitikiaje?



- "Hapana!"
- "Labda."
- "Sawa."



► Kwa nini unafikiri wangeitikia hivyo?

► Hata ikiwa itachukua muda, utafanya nini ili kuwaondolea hangaiko hilo? (Dokezo: Unayotenda ni muhimu zaidi kuliko unayosema.)

► Unafikiri hangaiko kuu la wazazi wako ni nini?

► Wazia wewe ni mzazi wa kijana fulani. Ungemwekea sheria kama hiyo? Ikiwa ndivyo, ungemwekea sheria gani na kwa nini?

WAZAZI WAKO WANAKUAMINI KWA KADIRI GANI?

Wazazi wako hawawezi kukuamini bila msingi wowote. Taja mambo fulani uliyofanya ambayo huenda yamepunguza kadiri ambayo wazazi wako wanakuamini.



Taja baadhi ya mambo ambayo umetenda yaliyowafanya wazazi wako wakuamini zaidi.



Je, una 'pesa' za kutosha katika 'akaunti' yako ya uaminifu zitakazokuwezesha kuzungumza na wazazi wako sasa—au usubiri?



Ikiwa unaona ni afadhali usubiri, basi unaweza kufanya nini ili kuongeza 'pesa' katika 'akaunti' yako ya uaminifu?

DOKEZO: Waonyeshe wazazi wako daftari uliloandika majibu yako, na ulitumie kama msingi wa mazungumzo yenu.

Utakapozungumza na wazazi wako, kumbuka kwamba Biblia inasema hivi: "Jibu, linapokuwa la upole, hugeuza ghadhabu, lakini neno linaloumiza hufanya hasira ipande."
—Methali 15:1.



JE, WAJUA? Kanuni zilizopo katika zoezi hili, zinaweza kukusaidia kuzungumza na mwajiri wako kuhusu sheria zilizowekwa katika sehemu ya kazi.

"Kutii sheria za wazazi wako ni kama kulipa mkopo wa benki, kadiri unavyolipa kwa wakati ndivyo unavyoaminika zaidi."—Kutoka katika kitabu *Maswali Ambayo Vijana Huuliza* —*Majibu Yafanyayo Kazi*, Buku la 2.